TANGAZO LA SERIKALI NA. 872 la tarehe 18/10/2024

SHERIA YA MAMLAKA NA MAJUKUMU YA MSAJILI WA HAZINA,
(SURA YA 370)

# HATI YA MABADILISHANO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(2))*

HATI YA MABADILISHANO YA ARDHI ILIYOPO ENEO LA KWALA WILAYA YA KIBAHA MKOA WA PWANI KATI YA SHIRIKA LA RELI TANZANIA NA HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBAHA YA MWAKA 2024

Sura ya 370 na Sura ya 257

KWA KUWA, kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina ikisomwa pamoja na Sheria ya Mashirika ya Umma, mali zote za Serikali zimewekwa chini ya Umiliki wa Msajili wa Hazina;

Sura ya 370

KWA KUWA, Rais anaweza, kwa mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 7(2) cha Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, kumpa Msajili wa Hazina maelekezo ya kuondosha mali za uwekezaji au mali yoyote inayomilikiwa na Msajili wa Hazina chini ya udhamini;

NA KWA KUWA, Rais ameona kuwa ni kwa maslahi ya umma kwamba Kiwanja Namba 1, Kitalu “B” Kwala chenye ukubwa wa ekari 625 kinachomilikiwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC) kubadilishwa na kuwa chini ya umiliki wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha na Kiwanja Namba 1, Kitalu “G” Kwala chenye ukubwa wa ekari 502 (matumizi ya viwanda) na Kiwanja Namba 4, Kitalu “G” Kwala chenye ukubwa wa ekari 123 (matumizi ya maegesho ya magari) kinachomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha kubadilishwa na kuwa chini ya umiliki wa Shirika la Reli Tanzania;

HIVYO BASI, kwa amri ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeelekezwa kama ifuatavyo:

Jina

1. Hati hii itajulikana kama Hati ya Mabadilishano ya Ardhi Iliyopo Eneo la Kwala Wilaya ya Kibaha Mkoa wa Pwani Kati ya Shirika la Reli Tanzania na Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha ya Mwaka 2024.

Mabadishano ya ardhi

2.-(1) Kiwanja Namba 1, Kitalu "B" Kwala chenye ukubwa wa ekari 625 kinachomilikiwa na Shirika la Reli Tanzania, bila uthibitisho wa ziada na kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Hati hii, kinabadilishwa na kuwa chini ya umiliki na matumizi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha.

(2) Kiwanja Namba 1, Kitalu "G" Kwala chenye ukubwa wa ekari 502 na Kiwanja Namba 4, Kitalu "G" Kwala chenye ukubwa wa ekari 123 vinavyomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, bila uthibitisho wa ziada na kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Hati hii, vinabadilishwa na kuwa chini ya umiliki na matumizi ya Shirika la Reli Tanzania.

KWA AMRI YA RAIS

Dodoma,
2 Oktoba, 2024

MOSES M. KUSILUKA
*Katibu Mkuu Kiongozi*